# Tangazo: Timu ya ERM CVS Inakuja kufwanya uchunguzo ya kampuni Tenke Fungurume Mining

*Timu ERM CVS Inataka Kusikia yenye wakaji wa mu concession na wengine wasaidizi watasema!*

Leo, 13 Agosti 2025, kuna **timu ERM CVS** inajulisha ya kama tarehe **8-19 mwezi ya Septemba 2025**, na **mwezi ya Novemba pia tarehe 3-6**, itakuja hapa kampuni ya **Tenke Fungurume Mining**, jimbo la Lualaba mu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ku fanya kazi ya uchunguzo kufwatana na mipango ya **Initiative for Responsible Mining Assurance (IRMA).** ERM CVS ni timu inayojitegemeya, na yenye kufwanya uchunguzo kwa macho kufwatana na mipango ya IRMA.

Wakati ya kazi ya mwezi ya Septemba, pia na mwezi ya Novemba wachunguzi ya ERM CVS watachunguza ufwanyakazi ya ndani ya kampuni na ma kazi inayofwatana. Tena, watasikiya ile watu watasema – mtu yeyote ule anagusiwa vile karibu ao mbari kwa ma kazi ya kampuni: ni kusema watu wa hapa, wafanyakazi ya kampuni, na watu ya serkali.

Wakati uchunguzo inaisha, uso ya mwisho ya uchunguzo ya IRMA itatangazwa hapa na katika peji ya uchunguzo ya IRMA (ama published on the IRMA audit page). Ripoti itaonesha vile ERM CVS ilichunguza TFM kufwatana na maitaji yote 400+ ya IRMA Standard for Responsible Mining, na kwa nini ERM CVS ilipatiya TFM ile lama. Tena, ripoti itaonesha alama ya mafanikio: IRMA Transparency, IRMA 50, IRMA 75, or IRMA 100.

CMOC TFM inaweza kutumiya iyi uchunguzo kuboresha namna ya kufanya kazi. Watu wengine, kwa upeke wale wanagusiwa pia na wafwanya kazi, wanaweza kutumiya iyi ripoti ya uchunguzo ju ya kuzungumza na TFM na wengine kwa usawa zaidi ili kuboresha utendakazi kwa njia ambazo imestahili vema kwao.

<table>
<tr><td colspan="2">8-19 Septemba 2025 pia 3-6 Novemba 2025<br><br>Ujumbe yako itasaidiya timu ya wachunguzi ya ERM CVS kuona matokeo ya utendakazi ya TFM kwa wakaji wa hapa na kupima namna TFM anafwanya kazi kufwatana na utendakazi wa bora zaidi. ERM CVS inakualika ukuye kuzungumza na timu ya wachunguzi wakati watakuya kampuni, tena/ao uandike na utume ujumbe wako ku ERM CVS ju ya TFM.<br><br>Utumiye yafwatayo ili uombe ushiriki ao utume ujumbe. Mazungumzo ile inaweza kuwa mu Kifransa, Kiswahili, Kiingereza ao Kichina. Unaweza kuomba mazungumzo ya mtu moja kwa moja mbele ya 27 Octoba 2025. Ujumbe na mawazo lako ile imetolewa ku ERM CVS kufikiya 6 Novemba 2025 itaandikwa mu uchunguzo.</td></tr>
<tr><td>Kwa njia ya web: erm.com/ermcvs/services/sector-specific-certification-schemes/irma-stakeholder-feedback-form/<br><br>Kwa njia ya email: post@ermcvs.com<br><br>Simu: +27 10 596 3739</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="2">Mawazo na mazungumzo ni siri. Mazungumzo itafanywa pasipo wafanyakazi ya kampuni kuwepo. ERM CVS haitatoa jina ya wale wasema mawazo yao/wale wanazungumuza na TFM ao IRMA, wala kuoneshwa kwa kartasi ingine. Peke yake mawazo itaandikwa kwa kifupi mu ripoti ya uchunguzo ya mwisho.</td></tr>
</table>

**Kwa habari Zaidi kuhusu:**

- Uchunguzo ya TFM ao kujiandikisha kwa ujumbe mupia: responsiblemining.net/tfm
- Kampuni ya uchunguzo ya ERM CVS iliyokubaliwa na IRMA: ermcvs.com
- Shaba ya IRMA, maitaji yake, kazi yake ya kipimo, ao uchunguzo ingine ya kampuni: responsiblemining.net
- Kujulisha malalamiko ju ya kazi ya uchunguzo: responsiblemining.net/complaints